

## Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA  
(DESIGN AND DRAWING)  
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA  
NA ROYAL DANISH EMBASSY  
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT  
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)

# MGAWANYO WA MALI YA NDOA



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA  
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

## MAANA YA NDOA

Ndoa maana yake ni Muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanarmke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa Maisha yao yote (Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kifungu cha 9).

## AINA ZA NDOA

Kuna aina tatu za ndoa:

A. Ndoa ya kidini

(i) Aina hii ya ndoa yaweza kuwa ni ndoa ya Kiislamu. aina hii ya ndoa huwa ni ndoa ya mke mmoja au zaidi ya mke mmoja (Mitala).

(ii) Ndoa ya Kikristo; Aina hii ya ndoa huwa ni ya mke mmoja tu.

B. Ndoa ya kiserikali; Aina hii ya ndoa huwa ni ya mke mmoja au idhaniwayo kuwa na mke zaidi ya mmoja

C. Ndoa ya kimila; Ndoa hii huweza kuwa ni ya mke mmoja au idhaniwayo kuwa na nike zaidi ya mmoja.

Pamoja na aina za ndoa zilizotajwa juu sheria ya ndoa inachukulia kwamba iwapo itathibitishwa kwamba mwanamume na mwanamke wameishi pamoja kwa muda wa miaka miwili au zaidi na kupata heshima ya mume na mke basi itakuwepo hoja ya kubishaniwa kwamba watu hao walioana ipasavyo. Madhumuni ya dhana hii ni kumwezesha mwanamke na watoto kupata masurufu pale ambapo ndoa inavunjwa.

## WAJIBU WA MUME AU MKE

Katika ndoa mume anao wajibu wa kumkimu mkewe kwa kumpatia malazi, Nguo na chakula, na mke mwenye kipato vile vile anao wajibu wa kumkimu mumewe ikiwa mume huyo:

- Hajimudu kabisa.
- Hawezi kupata chumo la Maisha yake kwa sababu ya athari ya akili au afya mbaya (Sheria ya ndoa 1971 kifungu 63).

## KUMILIKI MALI

Mke ana haki ya kumiliki Mali binafsi. Mali hiyo inaweza ikawa mali aliyopata kabla ya Ndoa na hata baada ya Ndoa kama ameipata kwa fedha zake mwenyewe. Pia Mke na Mume wanaweza kukubaliana kuwa mali ambayo kila mmoja alikuwa nayo kabla ya ndoa au wakati wa ndoa iwe yao kwa pamoja.

## MALI ILIYOPATIKANA WAKATI WA NDOA

Mali ya mke au mume iliyopatikana kutokana na jasho lao wote wawili ni mali yao kwa pamoja hata kama juhudi zao au jasho lao katika kupata hizi mali si sawasawa.

## KUGAWANA MALI

Dhana hii ya kugawana mali inajitokeza kati ya Mume na Mke baada ya ndoa kuvunjika kisheria.

Baada ya Mume na Mke kuachana kwa amri ya mahakama, Mume na Mke wanatakiwa kugawana mali yoyote waliyoipata wakati wa ndoa kwa juhudi zao za pamoja.

Wakati wa kugawana mali, ni lazima Mahakama iwe imejiridhisha na mambo yafuatayo:

- Kuwa mali inayogawiwa iwe imepatikana kutokana na juhudi za pamoja za mke a mume.
- Kuwa mali inayogawiwa ime-tokana na kuwepo kwa ndoa (Matrimonial Assets).
- Kwamba mali inayogawiwa imechumwa wakati ndoa inadumu.

Mchango wa mke katika kuchuma mali ni pamoja na kazi za ndani ambazo zinafanywa na mke wakati ndoa inaendelea.

Kama ilivyoamriwa katiaka kesi ya Bi HAWA MOHAMED DHIDI YA ALLY SEFU. Kuwa kwa kutunza nyumba wakati mumewe yuko safarini ilikuwa ni mchango tosha wa kumwezesha kupata sehemu ya mali iliyochumwa wakati wa ndoa.